

6

KIPO NINI BAADA YA KABURI?

Yesu Kristo huwaokoa watu wake kutoka hofu ya kifo. Kwao inakuwa “ni afadhali kutokuwemo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana” (2Kor 5:8) “nikae na Kristo, maana ni vizuri zaidi sana” (Fil 1:23).

“Naam nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya, kwa maana wewe upo pamoja nami” (Zab 23:4).

Kwa wale wanaomkataa Yesu Kristo Biblia inasema atarudi katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana” (2The 1:8,9).

7

JE NI KWELI KUNA MBINGUNI?

Yesu aliwafunulia juu ya ukweli huu wa mbingu kuwa anakwenda kuandaa kwa ajili yetu. Yesu alisema, “Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi, kama sivyo, ningeliwaambia; maana

naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi, nanyi mwepo” (Yoh 14:1-3). Moja ya sababu kwa nini mimi ni Mkristo, ni kwa sababu nategemea kukutana na Mwokozi wangu uso kwa uso, na kumshukuru kwa upendo wote kwangu. Ninatazamia kuufurahia uzuri wa mbinguni, ambapo patakuwa nyumbani kwangu milele yote.



Ukitaka kujiunga na mafundisho ya Biblia kwa njia ya Posta tuandikie:

Maswali
saba
Muhimu

Maswali saba Muhimu 7

Baadhi ya maswali muhimu ambayo watu wamekuwa wakiuliza ni, “Muumbaji yukoje? Nifanye nini kuhusu dhambi zangu? Ninawezaje kushinda majaribu? Ninawezaje kumjua Mungu? Ni nini kusudi la maisha? Kipo nini kwa ajili ya wale wanaomkataa Yesu Kristo baada ya kaburi?” Maswali yote haya yamejibiwa katika Neno la Mungu lililoandikwa, Biblia na katika nafsi ya Bwana Yesu Kristo, ambaye ni Neno la Mungu Aliye Hai.

1

MUUMBAJI YUKOJE?

Yesu alijibu swali hili. Alisema, “Aliyeniona mimi amemwona Baba” (Yoh 14:9). “Mimi na Baba tu umoja” (Yoh 10:30). Wakati mtu anautazama uso wa Yesu, anaweza kusema “Nimemwona Baba”. Yesu alikuwa Mungu akijitokeza kwa sura ya mwanadamu. Yesu alimleta Mungu chini kwa wanadamu, na akawainua watu kwa Mungu.

2

NIFANYE NINI KUHUSU DHAMBI ZANGU?

Nilimsikia mtu akikiri maneno hayo katika redio. Watu wengi wanaishi chini ya mzigo na hukumu ya dhambi. Rafiki, kama moyo wako unalia kilio cha maneno kama hayo, ninazo habari njema kwa ajili yako. Kupitia mtu huyo, Yesu Kristo, “mnahubiriwa msamaha wa dhambi” (Mdo 13:38). “Akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake” (Kol 1:20).

Wakati fulani hata mimi nilikuwa kama mwana mpotevu aliyeelezwa katika Luka sura 15. Nilikuwa mbali sana na Mungu. Lakini nilipomgeukia Mungu kwa huruma alinisamehe bure dhambi zangu zote. Katika msalaba wa Kristo, dhambi zako zote zinaweza kusamehewa. Njoo kwake sasa, na utaanza kuujua utamu wa pendo lake na huruma yake.

3

NITAWEZAJE KUSHINDA MAJARIBU?

Unahitaji nguvu ya kushinda majaribu. Unamhitaji Mwokozi awezaye kuleta nguvu na faraja moyoni mwako. Yesu Kristo atakupa nguvu ya kuishi maisha mapya. Ni Mwokozi aliye hai. “Aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye” (Ebr 7:25).

4

NINAWEZAJE KUMJUA MUNGU?

Katika mioyo yetu tunapenda kuwasiliana na mtu aliye mkuu kuliko sisi. Mungu mwenyewe anaweza kuitosheleza hamu hiyo. Yesu Kristo atakuleta kwenye familia ya Mungu. “Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake” (Yoh 1:12).

5

NI NINI KUSUDI LA MAISHA?

Baada ya kuongoka kwa mtume Paulo alitumwa kulipeleka jina lake, na kuwageuza watu “waiache giza na kuelekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu” (Mdo 26 :18). Katika huduma hii ya furaha hata wewe unaweza kupata furaha iliyo kuu katika kutimiza mapenzi ya Mungu katika maisha yako.